Jamhuri ya Ireland

# KWA NINI DATA ZANGU BINAFSI ZINAPELEKWA KWENYE EURODAC?

Aina A

**WAOMBAJI WA ULINZI WA KIMATAIFA**



SWAHILI

## KWA NINI NAPOKEA KITABU HIKI CHA MAELEZO?

Umeomba ulinzi wa kimataifa, unaojulikana pia kama hifadhi, katika nchi hii.

Brosha hii inatoa maelezo zaidi kuhusu data ambayo itahifadhiwa na mamlaka na kwa muda gani.

## KWA NINI NI LAZIMA NITOE ALAMA ZA VIDOLE NA PICHA?

Mamlaka katika nchi hii zitachukua alama zako za vidole na picha yako. Data hii, pamoja na taarifa kuhusu utambulisho wako na taarifa nyingine muhimu, itatumwa kwenye hifadhidata ya Eurodac.

Eurodac inaunganisha makundi fulani ya watu ambao si raia wa nchi za EU+ na data fulani za kipekee kama alama za vidole na picha. Hifadhidata hii inatumiwa na nchi 31 za EU+ ambazo zinaweza kuchakata data yako ili kupata taarifa zako. Nchi za EU+ zimeorodheshwa mwishoni mwa brosha hii.

# KANUNI YA USIMAMIZI WA HIFADHI NA UHAMIAJI NI NINI?



Nchi za EU+ zilikubaliana kuhusu sheria ya kawaida inayoitwa Kanuni ya Usimamizi wa Hifadhi na Uhamiaji, ambayo husaidia kuamua ni nchi gani inapaswa kuchunguza maombi ya ulinzi wa kimataifa. Sheria hii pia inaruhusu nchi za EU+ kusaidiana ikiwa nchi moja itapokea maombi mengi sana kwa wakati mmoja.

Unahakikishiwa kwamba moja ya nchi za EU+ itachunguza ombi lako la ulinzi wa kimataifa, lakini huwezi kuchagua ni nchi gani ya EU+ itakayohusika. Nchi itakayochunguza ombi lako itaamuliwa kulingana na Kanuni ya Usimamizi wa Hifadhi na Uhamiaji.

Ikiwa utahamia nchi nyingine ya EU+ bila ruhusa na vidole vyako vitafanyiwa tena uchukuaji wa alama, data zako zote zilizohifadhiwa katika Eurodac zitaonekana na mamlaka ya nchi hiyo.

**Sasa uko nchini Jamhuri ya Ireland ambayo ni mwanachama wa Umoja wa Ulaya [EU+].**
**Nch wanachama wa EU+ ni:**

Nchi 27 wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU): Austria, Ubelgiji, Bulgaria, Kroatia, Saiprasi Jamhuri ya Czech, Denmark, Estonia, Ufini, Ufaransa, Ujerumani, Ugiriki, Hungaria, Italia, Latvia, Lithuania, Luksemburgu, Malta, Uholanzi, Poland, Ureno, Jamhuri ya Ireland, Romania, Slovakia, Slovenia, Uhispania, Uswidi na

Nchi nyingine 4: Iceland, Liechtenstein, Norway na Uswisi.

## NI TAARIFA GANI ZINAZOHIFADHIWA KATIKA EURODAC?



Taarifa zifuatazo huhifadhiwa kila wakati:

- lama zako za vidole
- picha ya uso wako
- majina yote unayotumia sasa au uliyowahi kutumia hapo awali
- tarehe yako ya kuzaliwa
- mahali pako pa kuzaliwa
- utaifa wako
- Jinsia yako
- nakala za hati za utambulisho au za kusafiria ulizotumia, zikipatikana, ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu uhalali wake
- kitambulisho cha mtumishi aliyechukua alama zako za vidole na picha yako na tarehe data zako zilipokusanywa na kutumwa
- nchi uliyoomba ulinzi wa kimataifa
- tarehe ya ombi la ulinzi wa kimataifa.

Taarifa zifuatazo pia zitahifadhiwa katika Eurodac inapohitajika:

- nchi inayohusika na kuchunguza ombi lako
- kama umehamishwa, nchi ya EU+ ya kuhamishiwa
- kama ombi lako lilikataliwa na huna haki ya kubaki katika nchi za EU+
- kiwa ombi lako lilichunguzwa chini ya utaratibu wa mpakani na kukataliwa au ombi lako limechukuliwa kuwa limeondolewa
- taarifa kuhusu viza zozote zilizotolewa kwako na nchi ya EU+
- taarifa kuhusu wakati wowote ulpotoroka katika eneo la nchi za EU+
- taarifa kuhusu kama ulikubali ofa ya kurudi kwa hiari nchini kwako.

Una haki ya kupata na kurekebisha taarifa zisizo sahihi zilizohifadhiwa katika Eurodac na kuomba kufuta taarifa zako ikiwa zimeshughulikiwa kinyume na sheria. Unaweza kuwasiliana na msimamizi wa data kufanya hivyo. Maelezo ya mawasiliano ya msimamizi wa data yanaweza kupatikana katika brosha yenye jina **'Unachohitaji kujua kuhusu Eurodac'.**

## TAARIFA ZANGU BINAFSI ZITAHIFADHIWA KIWANGO CHA MUDA GANI KWENYE EURODAC?



Taarifa zako zitahifadhiwa kwa miaka 10 na kisha zitafutwa kiotomatiki.Ikiwa utapata uraia katika nchi ya EU+ kabla ya kuisha kwa kipindi hiki, data zako zitafutwa. Ikiwa data zako zitafutwa, hii haitaathiri hadhi yako katika nchi uliyopata uraia.

## JE, KUNA TAARIFA NYINGINE YOYOTE INAYOHIFADHIWA KATIKA EURODAC?

Matokeo ya ukaguzi wako wa usalama yatahifadhiwa ikiwa mamlaka zitabaini kuwa unaweza:

- kuwa na silaha
- kuwa mkatili
- kuwa umehusika katika uhalifu wa kigaidi
- kuwa umefanya uhalifu mkubwa ambao unaweza kukamatwa kwa ajili yake katika nchi nyingine ya EU+.

Katika kesi kama hizo, itachukuliwa kuwa unaweza kuleta tishio kwa usalama wa ndani. Hii itahifadhiwa katika Eurodac pamoja na sababu inayotumika au sababu zilizotajwa kwa kina hapo juu.

Ikiwa nchi za EU+ hazitakuona tena kama tishio kwa usalama wa ndani, taarifa hizi zitafutwa.

Una haki ya kupata na kurekebisha taarifa zisizo sahihi zilizohifadhiwa katika Eurodac na kuomba kufuta taarifa zako ikiwa zimekushughulikiwa kinyume na sheria. Unaweza kuwasiliana na mdhibiti wa data kufanya hivi. Maelezo ya mawasiliano ya mdhibiti wa data yanaweza kupatikana katika brosha yenye jina **'Unachohitaji kujua kuhusu Eurodac'.**

Brosha hii itatumiwa kwa madhumuni ya taarifa pekee. Haileti haki wala wajibu wowote. EUAA au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya EUAA hawawajibiki kwa matumizi yanayoweza kufanywa ya taarifa zilizomo katika brosha hii.

© Shirika la Umoja wa Ulaya la Hifadhi, 2025